



Rudi kaswali, kwani wewe hujaswali

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: Ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliingia msikitini kisha akaingia mtu mmoja, akaswali, kisha akamsalimia Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akajibu salamu, na akasema: "Rudi kaswali, kwani wewe hujaswali", akarudia kuswali kama alivyoswali mwanzo, kisha akaja, akamsalimia Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akasema: "Rudi kaswali kwani wewe hujaswali" (akafanya hivyo) Mara tatu, akasema: "Namuapa yule aliyekutuma kwa haki, siwezi kuswali vizuri zaidi ya hivyo, basi naomba nifundishe, akasema: "Utakaposimama katika swala basi toa takbira (sema: Allaahu Akbaru), kisha soma kiasi chepesi ulichonacho katika Qur'ani, kisha rukuu mpaka utulizane ukiwa umerukuu, kisha nyanyuka mpaka ulingane wima, kisha sujudu mpaka utulizane ukiwa umesujudu, kisha nyanyuka mpaka utulizane ukiwa umekaa, na ufanye hivyo katika swala yako yote".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Aliingia Mtume rehema na amani ziwe juu yake msikitini, akaingia baada yake mtu mmoja akaswali raka mbili haraka haraka, na hakutulizana katika kisimamo chake na rukuu yake na sijida yake, na alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake akimfuatilia katika swala yake, akaja kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake akiwa kaka pembezoni mwa msikiti, akamsalimia, akajibu salamu, na akasema kumwambia: Nenda karudie swala; kwani wewe hujaswali. Akarudi na akaswali haraka kama alivyoswali mwanzo, kisha akaja akamsalimia Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akasema kuwambia: Rudi kaswali; kwani wewe hujaswali, alifanya hivyo mara tatu. Yule bwana akasema: Namuapa yule aliyekutuma kwa haki, siwezi kufanya vizuri zaidi ya hivyo, basi nifundishe, akasema rehema na amani ziwe juu yake: Utakaposimama katika swala basi toa takbira ya kuhirimia swala, kisha soma mama wa Qur'ani (Suratul-Faatihah) na kile atakachotaka Mwenyezi Mungu ukisome, kisha rukuu mpaka utulizane ukiwa umerukuu kwa kuweka viganja vyako juu ya magoti yako na unyooshe mgongo wako na umakinike katika rukuu yako, kisha nyanyuka na unyooshe mgongo wako mpaka mifupa irudi katika viungo vyake na ulingane sawa ukiwa wima, kisha sujudu mpaka utulizane ukiwa umesujudu kwa kuliweka sawa paji la uso na pua, na mikono miwili na magoti mawili na ncha za vidole vya miguu miwili juu ya ardhi, kisha nyanyuka mpaka utulizane ukiwa umekaa kati ya sijida mbili, kisha fanya hivyo katika kila raka ndani ya swala yako.

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

